**KESI YA KIKATIBA INAYOPINGA MUUNDO WA KAMATI YA MAADILI YA MAWAKILI IMESIKILIZWA LEO MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

Mahakama Kuu ya Tanzania (Masjala Kuu) Dodoma imesimamisha kusikilizwa kwa mashauri mawili (2) ya kinidhamu yaliyoko kwenye Kamati ya Maadili ya Mawakili dhidi ya Wakili Peter Michael Madeleka mpaka hapo shauri la Kikatiba Namba 7817 la mwaka 2024 litakaposikilizwa na kutolewa uamuzi. Amri hiyo ya Mahakama imetolewa na jopo la Majaji watatu: Mhe. Jaji I. Mugeta, Mhe. Jaji S. Magoiga na Mhe. Jaji J. Masabo.

Tarehe 25 Januari na 11 Machi 2024 Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliwasilisha mbele ya Kamati ya Maadili ya Mawakili malalamiko / mashauri mawili ya kinidhamu dhidi ya wakili Peter Michael Madeleka, (Maombi Namba 02 na namba 07 ya mwaka 2024), akiiomba kamati iondoe jina la Peter Madeleka kwenye orodha ya mawakili.

Wakili Madeleka chini ya usimamizi wa mawakili kutoka Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) wakiongozwa wa wakili John Seka, alifungua kesi ya kikatiba Namba 7817 ya mwaka 2024 kupinga vifungu namba 4[1][b]; 4[3]; 4[4]; [ 4[5]; 4[6]; 5 and 10 vya Sheria ya Mawakili ambavyo vinaeleza muundo na namna ya usikilizwaji wa mashauri dhidi yake kwenye Kamati ya Maadili ya Mawakili.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndio mwenye mamlaka kisheria kuitisha vikao vya Kamati ya Maadili ya Mawakili. Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mjumbe wa Kamati ya Maadili ya Mawakili lakini pia ni mlalamikaji dhidi ya Madeleka kwenye Kamati hiyo. Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kuwakilishwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali endapo yeye hatakuwa mjumbe. Lakini kumbuka Naimbu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni Msaidizi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mjumbe mwingine ni Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini ambaye pia kwa mujibu wa Sheria, ni sehemu ya ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hivyo, wajumbe wote hawa watatu wanatoka ofisi moja (Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali).

Lakini pia msingi wa maombi namba 02 ya mwaka 2024 ni kutokana na maneno aliyodaiwa kuyatamka wakili Madeleka baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini kuwasilisha nia ya kuifuta kesi ya Hashimu Ally dhidi ya Pauline Gekul katika Mahakama ya Wilaya ya Babati na Mahakama kumkubalia na hatimae kesi hiyo kufutwa.

Kutokana na muundo wa Kamati kama ilivyoelezwa hapo juu, wakili Peter Michael Madeleka alifungua kesi Mahakama Kuu akiieleza Mahakama kuwa hatatendewa haki mbele ya Kamati hiyo na hivyo kuiomba Mahakama kusimamisha usikilizwaji wa mashauri mawili (Maombi Namba 02 na namba 07 ya mwaka 2024).

Pia wakili Madeleka anaamini kuwa endapo usikilizwaji ungefanyika kwenye Kamati ya Maadili ya Mawakili kuna uwezekano mkubwa wa uvunjwaji wa haki zake za msingi zilizopo katika Ibara ya 13[1], 13[2], 13[3], 13[6][a], 26[1], 29[1] na 29[2] ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Imetolewa na**

**Watetezi Tv**

**Dar es Salaam, Tanzania**

**30.04.2024**